



Hatoingia motoni mtu aliyeshududia vita vya Badri na Hudaibia

Kutoka kwa Jaabir radhi za Allah ziwe juu yao yeye na baba yake, amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu rehema na amani ziwe juu yake: "Hatoingia motoni mtu aliyeshududia vita vya Badri na Hudaibia".

[Sahih] [Imepokelewa na Ahmad]

Ameeleza Mtume rehema na amani ziwe juu yake ya kwamba hatoingia motoni aliyahuduria vita vya Badri vilivyotokea katika mwaka wa pili wa Hijiria (kalenda ya kiislamu) akipigana pamoja na Mtume rehema na amani ziwe juu yake, wala aliyahuduria suluhu ya Hudaibia, na ndani yake kukiwa na uungaji mkono wa ridhaa (Baiatu ridhiwani) uliotokea katika mwaka wa sita wa Hijiria.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/11148>

